JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALAZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA

30.08.2023

Mwenyekiti,
Waheshimiwa Wajumbe wote,
Baraza la Madiwani,
Halmashauri ya Wilaya ya Chunya

TAARIFA YA HESABU ZA MWISHO HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI 2023 KWENYE MKUTANO MAALUM WA BARAZA LA MADIWANI TAREHE 30/08/2023

1. **UTANGULIZI**

Kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa ya 1982 kifungu Na. 40 kama kilivyorekebishwa mwaka 2000. Halmashauri nchini zinapaswa kufunga hesabu na kuwasilisha kwa mdhibiti na Mkaguzi mkuu wa hesabu za serikali(CAG) si zaidi ya tarehe 30/09 ya kila mwaka.

Kazi ya ufungaji mahesabu ya mwaka 2022/2023 ilianza 10 Julai, 2023 na inategemewa kukamilika tarehe 31 Augosti 2023 kama ilivyoelekezwa na Serikali kwamba hesabu za mwaka 2022/2023 ziwasilishwe mapema kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili Mkaguzi aweze kuzikagua na kama kutakuwa na marekebisho yafanyike mapema na inapofika tarehe 30 Septemba 2023 hakuna marekebisho yatakayopokelewa tena.

Katika hesabu hizi Mfumo wa Ufungaji hesabu wa Kimataifa ujulikanao kama (IPSAS International Public Sector Accouting Standards - Accruals Basis) ndiyo uliotumika katika uandaaji wa hesabu za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

Uandaaji wa hesabu kuishia 30/06/2023 umezingatia Sheria za Fedha, Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2011, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982

kama ilivyorekebishwa mwaka 2000, miongozo inayotolewa na Bodi ya Uhasibu, Sera za Nchi, miongozo mbalimbali ya Serikali na Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

2. TAARIFA ZA HESABU ZA MWAKA 2022/2023

Taarifa za hesabu ya Halmashauri zimegawanyika katika maeneo makuu manne yafuatayo:-

a) Taarifa mbalimbali za Halmashauri (Council information)

b) Ripoti ya Halmashauri ya Hesabu ya mwaka 2022/2023 (District Councilors Report)

c) Taarifa za Hesabu ya mwaka 2022/2023 (Financial Statements):

- Mizania ya mahesabu (Financial Position),
- Mapato na Matumizi (Financial Performance),
- Mtiririko wa Fedha (Cash flow),
- Mwenendo wa rasilimali za Halmashauri (Statement of changes in net assets),
- Mapato na Matumizi ki-idara (Financial performance by function of the council),
- Malinganisho ya Mapato na Matumizi kati ya bajeti na hali halisi kwa kasma (statement of comparison of budget and actual by nature),
- Malinganisho ya mapato na matumizi kati ya bajeti na hali halisi kwa kila Idara (Statement of comparison of budget and actual by function).

d) Maelezo yanayohusu hesabu ya Halmashauri

MUHTASARI WA TAARIFA ZA HESABU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.

1. TAARIFA MBALIMBALI ZA HALMASHAURI (COUNCIL INFORMATION).

Masuala yanayohusu taarifa za Halmashauri ni:-

- Anuani ya Halmashauri,
- Mahali ilipo ofisi,
- Benki zinazotoa huduma kwa Halmashauri,
- Taarifa ya Mkurugenzi wa Halmashauri,
- Mwanasheria wa Halmashauri,
- Wakaguzi wa Mahesabu ya Halmashauri

2. TAARIFA YA HALMASHAURI YA HESABU ZA MWAKA 2022/2023 (DISTRICT COUNCILORS REPORT)

a) Maelezo ya Utangulizi wa uwasilishaji wa hesabu kuishia 30/06/2023:

(i) Dira ya Halmashauri:

Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ingependa kuwa na wakazi wenye maisha bora na endelevu kiuchumi na katika huduma za Jamii.

(ii) Dhima ya Halmashauri:

Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kwa kushirikiana na wadau na wahisani inalenga kutoa huduma bora na endelevu kwa wakazi wake ili kupunguza Umasikini na kuinua kipato.

(iii) Malengo ya Halmashauri

- Kupunguza maambukizi mapya ya UKIMWI na kuboresha utoaji wa huduma.
- Kuboresha,kuendeleza na kutekeleza kikamilifu Mpango wa Taifa wa kupambana na Rushwa
- Kuhakikisha huduma bora za kijamii zinawafikia Wananchi walio wengi na zilizoboreshwa.
- Kuboresha huduma za kiuchumi na kuimarisha miundombinu.
- Kuimarisha masuala ya utawala bora
- Kuhakikisha kuwepo kwa Usawa wa Kijamii,Kijinsia kuwawezesha na kushirikisha wananchi katika kujiletea maendeleo yao
- Kuboresha mfumo wa kukabiliana na dharura na majanga

(iv) Majukumu ya Halmashauri

Majukumu ya Halmashauri ya Wilaya yameainishwa ndani ya sheria ya Serikali za Mitaa yamwaka 1982 na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 145 na 146 ya mwaka 1977.

Baadhi ya Majukumu ni:-

a) Kuhakikisha kuwepo kwa Amani, Utulivu na Utawala Bora,
b) Kuhakikisha uwepo wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Kiuchumi,
c) Kwa kuzingatia Sera ya Kitaifa na Mipango ya Maendeleo Mjini na Vijiji kuwaletea wananchi Maendeleo ya Kiuchumi,
d) Kulinda na kuhifadhi rasilimali za Umma,
e) Kuendeleza Kilimo, Biashara na Viwanda,
f) Kuleta Maendeleo ya Elimu, Afya, Jamii, Utamaduni na Ustawi wa Jamii,
g) Kupunguza umaskini wa makundi yote ya Jamii kama vile Vijana, wanawake,Wazee na Walemavu.
h) Kupiga vita Umaskini, Maradhi na Ujinga,
i) Kuleta usawa katika ngazi zote za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kisiasa, kiuchumi, na kijamii.
j) Kubuni na kusimamia vyanzo vya mapato vya Halmashauri ili kuwezesha Halmashauri kutekeleza majukumu yake na kuongeza uwajibikaji katika masuala ya fedha,
k) Kusimamia Demokrasia na maamuzi ya wananchi,
l) Kutoa huduma zenye tija, gharama nafuu na kuhimiza ushirika kwa vikundi na watu wake,
m) Kutambua na kuendeleza masuala ya kijinsia,
n) Kuhifadhi na kuendeleza matumizi bora ya hifadhi ya mazingira

3. UHAI WA HALMASHAURI: (Going Concern)

Halmashauri ya Wilaya ya Chunya inategemewa kuwepo na kuendelea kutekeleza majukumu yake. Mamlaka inaendelea kuwepo daima

4. WAHESHIMIWA MADIWANI

Orodha ya majina ya Waheshimiwa Madiwani wanaounda Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kisheria, orodha hii inaonyesha Waheshimiwa waliokuwepo mwaka 2020/2021 hadi mwaka 2022/2023 ulipoisha.

Kuna Waheshimiwa Madiwani wa kuchaguliwa **20**, Waheshimiwa Madiwani wa Viti Maalum ni **7** na Waheshimiwa Wabunge 2, Mheshimiwa mmoja ni wa Jimbo na mwingine ni mheshimiwa Mbunge Viti Maalumu na kufanya Baraza kuwa na wajumbe **29.**

5. USTAWI WA WATUMISHI WA HALMASHAURI

Halmashauri ya Wilaya ya Chunya inaamini watumishi wanafanya kazi kwa kujituma na kutumia uzoefu wao. Hakuna ubaguzi wa kikabila,kijinsia, ulemavu au kidini, wote ni sawa Mwajiri huchangia 15% ya mshahara wa mtumishi katika mifuko mbalimbali ya hifadhi ya jamii na mtumishi huchangia 5% ya mshahara wake. Watumishi hupata huduma za afya na matibabu kupitia Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) na bajeti inayotengwa na Halmashauri.

6. WAJIBU WA BARAZA LA MADIWANI

Sheria ya Serikali za Mitaa ya 1982, kifungu 40 kinaagiza Halmashauri kuandaa hesabu zake zitakazo onyesha Ustawi na mwenendo unaostahili wa mahesabu, matumizi ya Kanuni za Fedha za Serikali za Mitaa (LAFM) ya 2010, kifungu 31(7) kinasisitiza suala hili.

Taarifa hii inathibitisha kwamba hesabu zimeandaliwa kwa kuzingatia Sera na sifa zingine za kitaalamu. Hesabu hizi zimethibitishwa na kamati ya Wataalam wa Halmashauri **(CMT)** na kamati ya Ukaguzi kwamba zimeandaliwa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Ufungaji wa Hesabu ("International public sector accounting standards" - IPSAS) na kwamba mamlaka hii itaendelea kuwepo.

Aidha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango imetimiza wajibu wake kama ifuatavyo:-

i) Kusimamia mamlaka ili kuhakikisha kumbukumbu za hesabu zinatunzwa vizuri na zinathibitisha hesabu zimezingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali.

ii) Kusimamia mamlaka kwa kuhakikisha rasilimali za Halmashauri zinatunzwa na hakuna namna yoyote ya upotevu, uharibifu wa rasilimali.

iii) Kusimamia Sheria ya manunuzi ya Na. 7 ya 2011 na kanuni zinginezo.

iv) Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango inatoa mapendekezo kwa Baraza la Madiwani kuridhia Hesabu hizi ili ziwasilishwe kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa Sheria.

Mhe. Mwenyekiti,

Naomba kuwasilisha hesabu za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kwa mwaka fedha 2022/2023 kama ifuatavyo.

1. Mizania ya mwaka 2022/2023 (Financial Position)

Mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2023 rasilimali za Halmashauri za muda mrefu na mfupi zilikuwa na thamani ya jumla ya **TZS. 43,969,280,086/=** ukilinganishwa na mwaka 2021/2022 ambapo zilikuwa **TZS.34,993,864,486/=** ongezeko la rasilimali za Halmashauri limetokana na Halmashauri kutekeleza miradi mbalimbali yenye mwelekeo wa rasilimali za kudumu pamoja na ununuzi wa vifaa na mitambo, ujenzi wa nyumba, madarasa na vyoo.

2. Taarifa ya mapato na matumizi kwa mwaka 2022/2023

(i) Halmashauri ilikusanya kutoka kwenye vyanzo vyake (own source) jumla ya **TZS. 6,279,902,160.35** sawa na asilimia **117.81** ya makisio ya mwaka TZS **5,330,600,000.00** kwenye vyanzo vifuatanyo:

(a) Mapato halisi (Own source proper) **TZS. 4,580,565,265.54** sawa na asilimia **105.69** ya makisio ya **TZS. 4,334,000,000.00**

(b) Mapato lindwa (Protected) **TZS. 1,699,336,894.81** sawa na asilimia **170.51** ya makisio ya **TZS. 996,600,000.00**

(ii) Fedha za ruzuku na wafadhili tumepokea jumla ya **TZS. 28,407,207,490.83** kama ifuatavyo:

a) Matumizi mengineyo tumepokea **TZS. 885,917,345.50** sawa na asilimia **119.12** ya makisio ya **TZS.743,712,000.00**

Hizi ni fedha za OC proper, Ruzuku ya mitihani, likizo za walimu na fedha za uhamisho.

b) Fedha za mishahara tumepokea **TZS. 14,634,317,145.33** sawa na asilimia **113.56** ya makisio ya **TZS. 12,886,973,000.00**
Fedha hizi zinajumuisha mishahara halisi na mchango wa mwajiri kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.

c) Fedha za miradi ya maendeleo tumepokea **TZS.8,764,558,616.26** sawa na asilimia **97** ya makisio ya **TZS. 8,947,823,000.00** Fedha hizi zimepokelewa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kama mfuko wa Afya wa Pamoja (Basket fund), Elimu bure,TASAF,Ukarabati wa vituo vya Afya, Hospitali ya wilaya, Umaliziaji ofisi ya Halmashauri, Nyumba ya Mkurugenzi, UNICEF, CDCF, Chanjo ya Rubela, umaliziaji wa maboma, Waltereed, EP4R msingi na Sekondari, Swash (DFID)

3. Taarifa ya Mtiririko wa fedha kwa mwaka **2022/2023**
Mtiririko wa fedha kwa kuanzia kiwango cha ziada/bakaa ya mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2023 ilikuwa kama ifuatavyo:-

Mapato

Salio anzia tarehe 1/07/2022…… **TZS.** 493,205,728.00

- Kiasi kilichopokelewa

Mapato ya ndani…….. **TZS.** 4,580,565,265.54
Ruzuku matumizi mengineyo .. **TZS.** 15,520,234,490.70
Ruzuku ya maendeleo…… **TZS.** 8,764,558,616.26

Jumla ya mapato yote…… TZS**. 28,865,358,372.71**

Matumizi

Mishahara Pamoja na matumizi mengineyo TZS. 17,728,782,515.31
Matumizi ya fedha za mapato ya ndani TZS. 4,580,565,265.54
Matumizi miradi ya maendeleo ya ruzuku TZS. 4,566,227,336.86

Jumla ya Matumizi yote…… TZS. 26,875,575,117.71

Salio/Bakaa iliyokuwepo benki 30/6/2023 TZS. 1,989,783,255.00

Mhe,Mwenyekiti,

Maelezo ya hali ya fedha

a. MIZANIA(Financial Position)

1. **Fedha taslimu (Cash and Cash Equivalents)**

Fedha taslimu imeongezeka kutoka **TZS 493,205,727** mwaka **2021/2022** mpaka **TZS 1,989,783,255** mwaka **2022/2023**, ongezeko hili ni sawa na asilimia **303.44** ukilinganisha na mwaka jana. Hii inatokana na mapokezi ya fedha za mradi maendeleo nje ya bajeti kama mfuko wa Afya wa Pamoja (Basket fund), ujenzi wa miundombinu ya shule (BOOST).

2. **Wadaiwa (Receivable)**

Wadaiwa wamepungua kutoka **TZS. 249,886,626** mwaka 2021/2022 mpaka **TZS. 213,489,067** ya mwaka 2022/2023. Hii imesababishwa na kupungua kwa deni tunalodai la Vibanda vya Sokoni, Ushuru wa Madini na Masurufu ya watumishi.

3. **Mali Ghalani. (Stock/Inventories**)

Mpaka tunafunga hesabu za mwisho kulikuwepo na madawa, yenye thamani ya **TZS. 234,509,000.00**

4. **Wadai (payables**)

Miongoni mwa wadai wa Halmashauri ni madeni ya watumishi, wazabuni wa Halmashauri pamoja na makato ya kisheria kwenye taasisi za fedha. Kwa mwaka fedha unaoishia Juni 30 ,2023 jumla ya wadai wa Halmashauri **TZS. 74,848,838** madai haya yamepungua ukilinganisha na mwaka 2021/2022. Hii inatokana na kulipwa kwa madeni ya shule, kupunguza deni la PSSSF, deni la wanawake na vijana na wazabuni

b. MAPATO

1. Kodi mbalimbali

Mapato yatokanayo na kodi mbalimbali yamepungua kutoka **TZS 2,051,296,068** mwaka **2021/2022** mpaka **TZS. 1,850,531,263** kwa msimu wa **2022/2023.** Hii ni sawa na upungufu wa asilimia **10.84** lililotokana na mabadiliko ya kuhamishwa kwa ushuru wa Huduma kwenda kwenye kifungu cha Ada, Faini na Leseni.

2. Ada, faini, adhabu na leseni

Mapato kutokana na vyanzo hivi yameongezeka kutoka **TZS. 1,369,727,239** mwaka **2021/2022** mpaka **TZS 1,540,729,512** mwaka **2022/2023.** Hii ni sawa na asilimia **12.48** ukilinganisha na mwaka **2021/2022**

3. Thamani ya rasilimali zilizotumika (Depreciation)

Hii ni sehemu ya uchakavu wa majengo, mitambo na vifaa ambayo inajumuishwa kama sehemu ya mapato kwa kila mwaka baada ya kutumika hiyo rasilimali.

Kwa mwaka 2022/2023 thamani ya rasilimali iliyotumika ilikuwa **TZS 575,937,996**

c. MATUMIZI

1**. Mishahara,vibarua na Maslahi ya mwajiriwa**

Malipo ya mishahara na maslahi ya watumishi yameongezeka kutoka **TZS 13,273,420,230** mwaka 2021/2022 mpaka **TZS 13,546,702,705** ya mwaka 2022/2023 kutokana na malipo ya madai ya mishahara na baadhi ya watumishi kupanda madaraja.

2. **Ununuzi wa vifaa na gharama za kujikimu kwa wafanyakazi**

Ununuzi wa vifaa na gharama za kujikimu kwa watumishi imepungua kutoka **TZS. 6,383,443,858** mwaka 2021/2022 mpaka **TZS. 3,452,397,643** mwaka 2022/2023. Hii inatokana na fedha nyingi kuelekezwa kwenye miradi ya maendeleo na kupunguza matumizi ya kawaida.

3. Gharama za matengenezo

Matumizi ya gharama za matengenezo ni pamoja na matengenezo na magari na ununuzi wa mafuta ya kuendeshea mitambo, magari na pikipiki ambayo yamepungua kutoka **TZS. 2,664,378,306** mwaka 2021/2022 mpaka **TZS. 2,345,019,403** mwaka 2022/2023.

Upungufu huu unatokana na kuwepo kwa magari mapya ya usimamizi wa miradi mbalimbali hivyo kupunguza gharama ya matengenezo.

4. Ruzuku na michango ya kuchangia jamii

Kiasi kimepungua kutoka **TZS 1,324,554,260** mwaka 2021/2022 hadi **TZS** 437,175,200 mwaka 2022/2023. Hali hii imesababishwa na kuchelewa kuletwa kwa fedha za TASAF robo ya Nne.

Mhe. Mwenyekiti, Kutokana na mabadiliko ya tarehe za uwasilishaji wa hesabu, taarifa hii inawasilishwa mbele ya Baraza la Madiwani leo tarehe 30/08/2023 ili ipate Baraka kabla haijawasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali tarehe 31/08/2023.

Naomba kuwasilisha.

Tamim H. Kambona
Mkurugenzi Mtendaji (W)
CHUNYA